Serikali yakamilisha mafunzo ya Uraia na Utawala Bora ..Uk.3


tanzaniabora @tanzaniabora @tanzaniabora

# Tanzania BORA

Ni Mimi na Wewe

Tovuti: www.tanzaniabora.co.tz | ISSN 4256-1873 Toleo Na.16 Tanzania Bora JUMANNE Februari 04, 2025 Bei Tsh. 1,000 | Ksh. 100



Tanzania BORA MICHEZO

Mashabiki Simba watamba na timu yao

YANGA - POINT TATU ZA SIMBA TUNAZITAKA

PSG, ARSENAL ZATAJWA VITA YA GOMA

## MIAKA 48 CCM

# Dkt Samia, Dkt Mwinyi, Dkt Nchimbi kutambulishwa rasmi Dodoma J'tano

>> Makalla asema chama hicho kina mafanikio makubwa miaka yote kikiwa madarakani

>> Wana CCM, Wananchi wakaribishwa kuhudhuria sherehe hizo

>> Yajivunia kuwa na wanachama Milioni 12, kudumisha amani na utulivu wa nchi

Habari Uk. 2



## Serikali kumaliza Adha ya umeme nchini

NA MWANDISHI WETU

MATATIZO ya kukatika umeme yaliyokithiri katika maeneo mengi ya nchi yanaendelea kupatiwa ufumbuzi na serikali, ili kuhakikisha nishati hiyo inapatikana kwa uhakika.

Hayo yamebainishwa na Naibu Waziri wa Nishati, Mhe Judith

Inaendelea Uk. 3

# Biteko ataka umoja na mshikamano CCM

HABARI UK.2



# DKT SAMIA, DKT MWINYI, DKT NCHIMBI KUTAMBULISHWA..

NA MWANDISHI WETU

CHAMA Cha Mapinduzi CCM, kimetangaza rasmi kuwa wagombea wake wa Urais na Mgombea Mwenza kupitia chama hicho, watatambulishwa katika kilele cha sherehe za miaka 48 ya chama hicho zitakazofanyika Jijini Dodoma.

Wagombea hao ni pamoja na Mwenyekiti wa CCM na Rais wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan anayegombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mwingine ni Dkt. Husein Ali Mwinyi atakayepeperusha bendera ya CCM kugombea Urais wa Zanzibar.

Akizungumza na Waandishi wa Habari jijini Dodoma Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa CCM, CPA Amos Makalla alisema vilevile Mgombea Mwenza wa Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Emmanuel Nchimbi naye atatambulishwa katika sherehe hizo.

Makalla amemtaja mgeni rasmi kuwa ni Dkt Samia huku akiwaalika wanachama wa CCM na wananchi kuhudhuria sherehe hizo ambazo zinatarajiwa kufana kama ulivyofanyika Mkutano Mkuu wa CCM Januauri 18 na 19 jijini humo.

Alisema maaandalizi ya mkutano huo yanaendelea kukamilika, ambao pia utahudhuriwa na viongozi mbalimbali wa CCM pamoja na marafiki wa chama hicho.

"Hizi ni sherehe za CCM, hivyo siku hiyo tutawatambulisha wagombea wetu kwa wana CCM lakini siku ikifika tutawatambulisha kwa wananchi."

Makalla alisema CCM kinatimiza miaka 48 kikiwa ni chama imara kilichoaminiwa kushika dola kikiwa na wanachama 12 milioni hivyo kina dhamana na heshima kubwa.




# BITEKO ATAKA UMOJA NA MSHIKAMANO CCM

NA MWANDISHI WETU

WAKATI Chama Cha Mapinduzi CCM kikijiandaa kufanya sherehe za maadhimisho ya miaka 48 Jumatano ijayo jijini Dodoma, Naibu Waziri Mkuu ambaye pia ni Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Dkt. Doto Biteko ameonya uwepo wa makundi ndani ya chama hicho kuelekea uchaguzi, badala yake nguvu kubwa ielekezwe kwenye kujenga umoja na kutowapa nafasi wapinzani.

Dkt. Biteko amesema hayo katika mkutano wa Jimbo la Chamwino ulioendana na uwasilishaji wa utekelezaji wa ilani ya CCM katika kipindi cha maka mitano ya mbunge wa Jimbo hilo, Deogratius Ndejembi ambayo pia n Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

"Uchaguzi unaokuja ni uchaguzi usiokuwa wa majaribio ni uchaguzI unaotaka kuungana kwa pamoja na tulivyo wengi, tunaweza tukawa na tofauti mbalimbali na misimamo ya aina tofauti niwaombe tuache tofauti zetu tukitazame chama tushikamane kwa pamoja hatuna sababu ya kuhangaika kuwazungumza wengine tuzungumze mambo tuliyonayo ndani ya chama chetu," alisema Dkt. Doto Biteko.

Aidha Dkt. Biteko aliongeza kuwa "Nchi yetu ina vyama vingi vya siasa vina kazi mbili na chama kimoja kina kazi ya kufanya na chama kingine kina kazi ya kusema nyie wana CCM fanyeni kazi, hivyo vyama vingine viachieni maneno ya kusema wananchi watawapima kwa kazi sio kwa maneno."

# SERIKALI KUMALIZA ADHA YA UMEME NCHINI

NA MWANDISHI WETU

MATATIZO ya kukatika umeme yaliyokithiri katika maeneo mengi ya nchi yanaendelea kupatiwa ufumbuzi na serikali, ili kuhakikisha nishati hiyo inapatikana kwa uhakika.

Hayo yamebainishwa na Naibu Waziri wa Nishati, Mhe Judith Kapinga ambaye aliahidi serikali inahakikisha wananchi wanapata umeme wa uhakika na kwa ajili ya shughuli za maendeleo.

Kapinga aliyasema hayo jana Januari 03, 2025 Bungeni jijini Dodoma wakati akijibu swali la la Mbunge wa Lushoto Mhe. Shabani Shekilindi aliyetaka kufahamu ni lini Serikali itaondoa changamoto ya kukatika umeme katika Wilaya ya Lushoto kwa kuweka suluhisho la kudumu.

Alisema serikali itafuatilia kwa kipindi cha wiki moja ili kufahamu ni jambo gani linasababisha changamoto ya kukatika kwa umeme wilayani Lushoto.

"Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge iwapo kuna matengenezo tutahakikisha yanakamilika kwa haraka," alisisitiza Mhe. Kapinga

Akijibu swali Mbunge wa Nkasi Kusini, Mhe. Vicent Mbogo aliyetaka kufahamu uwepo wa nishati ya umeme katika Kijiji cha Msamba-Masokolo, Lyapinda, Izinga na Lyele na katika Vitongoji vya Kisenga na Lupata, Mhe. Kapinga amesema Wilaya ya Nkasi ina jumla ya vijiji 90 ambavyo vyote vimepatiwa huduma ya umeme vikiwemo vijiji vya Lyele na Lyapinda.

Aidha, amesema Kitongoji cha Lupata kilichopo katika Kijiji cha Lyapinda kitapata umeme kupitia mradi wa Vitongoji 15 vya Mbunge utakaotekelezwa na Mkandarasi aitwae M/s STEG International Services Ltd ambaye ameshakamilisha hatua za upimaji na usanifu.

NAIBU Waziri wa Nishati Judith Kapinga, amesema kwamba changamoto ya mgao wa umeme nchini itaisha rasmi mwezi wa Machi, mara baada ya mtambo namba 9 wenye uwezo wa kuzalisha megawati 235 kufanyiwa majaribio jana na mwingine utajaribiwa mwezi wa ujao, hali ambayo itaondoa adha ya umeme nchini.

Kauli hiyo aliitoa, Bungeni baada ya kuulizwa swali na Spika wa Bunge Dkt Tulia Ackson kwamba ni lini mgao wa umeme utamalizika katika taifa hili.

"Tuliahidi mwezi huu tuna ratiba ya kuzindua mtambo huu (mtambo no 9 katika mradi wa Bwawa la Julius Nyerere) na ratiba hii iko palepale, tunawashukuru sana.

# Ccm bagamoyo hapatoshi nafasi ya uenyekiti

NA MWANDISHI WETU

IDADI ya Wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wapatao 52 kutoka Wilaya ya Bagamoyo, Mkoani Pwani, wamejitokeza kuchukua fomu za kuwania nafasi ya Mwenyekiti wa chama hicho wilayani humo.

Hatua hii imechukuliwa kufuatia kuzibwa kwa nafasi hiyo baada ya Mwenyekiti wa awali, Alhaj Abdul Sharif Zahoro, kuondolewa kutokana na kukiuka maadili ya uongozi na Kamati Kuu ya CCM Taifa iliyofanya maamuzi hayo katika kikao maalum kilichofanyika tarehe 1 Septemba 2024.

Akizungumzia kumalizika kwa zoezi hilo, Katibu Mwenezi wa Wilaya ya Bagamoyo, Ramadhani Lukanga, alieleza kuwa zoezi hilo linahusisha kuchagua Mwenyekiti atakayechukua nafasi ya Abdul Sharif, ambaye ametenguliwa na uongozi wa CCM Taifa.

Alieleza, kati ya wanachama hao waliochukua fomu, 46 walirejesha fomu zao kabla ya kufika mwisho wa zoezi hilo tarehe 28 Januari mwaka huu.

"Kamati ya Siasa inawapongeza wanachama wote waliochukua fomu, wametimiza demokrasia, Hatua inayofuata ni kupanga tarehe ya kukutana ili kupitia majina ya wagombea kabla ya kuyapeleka Mkoani na Ngazi ya Taifa kwa ajili ya mchujo," alisisitiza Lukanga.

Lukanga alitoa wito kwa wanachama wa CCM wilayani Bagamoyo kuwa na utulivu na kuvuta subira wakati vikao vikipitia majina ya wagombea, baada ya hapo, uchaguzi wa kumpata mrithi wa nafasi hiyo utaandaliwa.

"Zoezi la uchukuaji wa fomu na mchakato mzima wa kuchuja na kupiga kura linahusisha wanachama wanaogombea pamoja na wapambe wao, Hivyo, tunawaasa wanachama baada ya vikao na kumtangaza Mwenyekiti mpya tuvunje makundi na kuendeleza umoja wetu," alisisitiza Lukanga.

Mwenyekiti aliyetenguliwa, Alhaj Abdul Sharif, aliiongoza CCM Wilaya ya Bagamoyo kwa vipindi viwili kabla ya Kamati Kuu ya CCM Taifa kuamua kumuondoa kwenye nafasi hiyo.

Viongozi wengine waliotenguliwa septemba 1 2024 ,ni pamoja na Paline Ninje, aliyekuwa Mwenyekiti wa UWT Lindi, na Munira Nkango, aliyekuwa Mwenyekiti wa UVCCM Singida.

# MAKALLA: CCM INAJIMUDU

NA MWANDISHI WETU

KATIBU wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa (NEC), Itikadi Uenezi na Mafunzo, CPA Amos Makalla amesema CCM haihitaji kubebwa kwani inabebwa na kuuzwa na kazi nzuri zinavyofanywa na madiwani, Wabunge na Rais Samia Suluhu Hassan.

"CCM inabebwa na kazi nzuri zinazofanywa na wabunge na madiwani wake, hivyo tunaimani CCM inauzwa na kazi nzuri iliyofanywa na waheshimiwa wabunge, madiwani na Mheshimiwa Rais, kwani kazi zake zinaonekana," amesema CPA Makalla.

Sambamba na hayo, Makalla amesema CCM wanatembea kifua mbele kwa ajili ya kiongozi wao ambaye ni mwenyekiti kitaifa Rais Samia Suluhu Hassan na 4R zake na fedha anazozitoa kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo nchini.

Akizungumzia maendeleo yaliyofanywa na serikali ya CCM katika jimbo hla Ukonga alisema maji safi ya bomba yalikuwa ni historia na hadithi za kusadikika kwa wananchi wa eneo hilo lakini mbunge wao kupitia tiketi ya CCM, Jerry Silaa aliwapigania kuhakiisha wanapata miradi ya maji safi.

Makalla ameongeza akiwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam alipata nafasi ya kusimamia ujenzi wa madarasa ya UVIKO na katika jimbo la Ukonga walipata bahati ya kupewa fedha nyingi kwa ajili ya ujenzi wa madarasa mengi zaidi kuliko majimbo yote.

Pia amesema mbali na elimu na maji kuna maendeleo makubwa katika sekta ya afya kwa ujenzi wa hospitali, zahanati na vituo vya afya katika kata mbalimbali na ujenzi wa mradi wa DMDP.




# Dkt Samia ndiyo mgombea stahiki-SUKI

NA WILLIUM PAUL, ROMBO

MJUMBE wa Kamati Kuu ya Chama cha Mapinduzi na Katibu wa Nec Siasa na Uhusiano wa Kimataifa (SUKI), Rabia Hamid amesema kuwa kilichofanywa na Wajumbe wa Mkutano mkuu kumpitisha Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwa mgombea wa Chama hicho katika uchaguzi Mkuu mwaka huu ni kwa mujibu wa katiba ya Chama.

Rabia ambaye ni mlezi wa Chama hicho mkoa wa Kilimanjaro alitoa kauli hiyo jana wakati wa maadhimisho ya miaka 48 ya kuzaliwa kwa Chama cha Mapinduzi ambapo kimkoa yamefanyika kata ya Katangara mrere wilayani Rombo.

Alisema kuwa, wapo baadhi ya wanasiasa ambao wamekuwa wkaipotosha kuwa kilichofanyika na Wajumbe hao ni kukiuka katiba ya chama na kuwataka wanaccm na wananchi kuwapuuza.

"Mkutano mkuu wa Chama cha Mapinduzi ndio chombo cha mwisho cha maamuzi na kilichofanywa na Wajumbe wake kimezingatia katiba ya Chama hivyo wapuuzeni hao wanaoibuka na kutoa taarifa za uongo" Alisema Rabia.

Mjumbe huyo wa Nec alisema kuwa, kwa sasa Chama hicho kinaenda kujipanga kuelekea uchaguzi mkuu wa 2025 ili kuhakikisha wagombea wake wanashinda kwa kishindo na Tanzania inaenda kuwa ya kijani.

Alisema kuwa, kwa sasa wameshawahesabu wapiga kura wa ccm na uchaguzi wa mwaka huu Chama kitaenda kushinda kwa kishindo na kuwataka Wapinzani kukaa mkao wa kula.

Rabia alisema kuwa, hakuna chama chenye historia kama CCM na uimara wake ambapo wananchi wamekuwa wakikituma kupitia viongozi wake na wao wapo tayari kutumwa na kuwatumikia wananchi.

Aliongeza kuwa, Kilimanjaro imebadilika katika swala la umoja upo vizuri na hana shaka katika uchaguzi wa 2025 chama kitashinda kwa kishindo ili kukuza nguvu na umoja kama Watanzania.

"Wananchi mnawajibu wa kumuongezea moyo wa kutafuta fedha nyingi zaidi za maendeleo kwa kumpa kura nyingi za kishindo pamoja na kuilinda na kuitunza miradi inayotekelezwa ili iweze kudumu muda mrefu.

Kwa upande wake, Mjumbe wa Halmashauri kuu ya CCM Taifa kupitia mkoa wa Kilimanjaro, Seleman Mfinanga alisema kuwa, miaka 48 ya kuzaliwa kwa chama hicho yapo mafanikio makubwa ya kujivunia katika kipindi chote hicho.

# Serikali yakamilisha mafunzo ya uraia na utawala bora

NA DOTTO KWILASA, MTWARA

WIZARA ya Katiba na Sheria imehitimisha kambi ya mafunzo na utoaji wa elimu ya uraia na utawala bora mkoani Mtwara kwa viongozi wa ngazi mbalimbali, kuanzia ngazi ya mkoa, wilaya, kata, hadi vijiji sambamba na kampeni ya msaada wa kisheria ya Mama Samia, iliyokuwa ikitoa huduma kwa wananchi katika halmashauri zote za mkoa huo.

Mafunzo haya yalilenga kuimarisha uelewa wa viongozi na wananchi kuhusu haki na wajibu wao katika utawala bora, sheria, na demokrasia.

Akizungumza na Waandishi wa habari mara baada ya kuhitimisha mafunzo hayo, Wakili wa Serikali Mkuu na Mratibu wa Mafunzo ya Elimu ya Uraia na Utawala Bora kutoka Wizara ya Katiba na Sheria, Prosper Alexander, ameeleza kuwa kwa jumla mafunzo hayo yameendeshwa kwa ufanisi na mafanikio.

Amesema kuwa mafunzo hayo yamefanikiwa kuyafikia makundi yote muhimu, ikiwa ni pamoja na Kamati za Usalama za mkoa, wilaya, na watendaji wa kata na vijiji.

"Tumefanikiwa kufika katika halmashauri zote tisa za wilaya hapa Mtwara. Tumeona wahusika wamefurahia mafunzo haya na wanatamani yawe endelevu. Wameahidi kutumia elimu waliyopata katika utekelezaji wa majukumu yao," amesema Alexander.

Aidha, amesema matarajio ya Wizara ni kuona matokeo chanya ya mafunzo hayo yakionekana katika jamii, ambapo viongozi na wananchi watakuwa na uelewa bora wa haki zao na utawala bora.

Naye, Wakili wa Serikali na Mratibu Msaidizi wa Mafunzo ya Elimu ya Uraia na Utawala Bora, Rhoda Longwe, amesema mafunzo hayo yamekuwa na tija kubwa kwani washiriki wamependekeza kuwa yafanyike katika mikoa yote nchini.

Longwe amebainisha kuwa mafunzo haya yameongeza ufanisi katika usimamizi wa sheria na utawala bora, hivyo kuweka misingi imara ya maendeleo endelevu katika mkoa wa Mtwara na maeneo jirani.

Naye Mrakibu Msaidizi wa Polisi na Mwanasheria wa Serikali, Nicholas Edward Mhagama, ameeleza kuwa mada ya ulinzi na usalama ni miongoni mwa mada zilizopewa kipaumbele katika mafunzo hayo, na kwamba mwitikio kutoka kwa washiriki umekuwa mkubwa.

"Baada ya mafunzo haya ni matumaini yangu kuwa kutakuwa na ushirikiano mkubwa baina ya vyombo vya usalama na jamii," amesema Mhagama.

Afisa Utumishi kutoka Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Agness Mabago, amesema kuwa mafunzo hayo yamegusa namna mamlaka kwa Umma inavyofanya kazi, na pia kuhamasisha ushirikishwaji wa wananchi wa chini katika maamuzi ya utawala.

"Mafunzo haya pia yatasaidia wananchi kujua haki na wajibu wao, ikiwa ni pamoja na matumizi sahihi ya sheria zilizowekwa na Serikali katika kufanya maamuzi," ameongeza Mabago.

Kwa upande wake, Afisa Uchunguzi kutoka Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Juliana Laurent, amesema kupitia watumishi waliopata mafunzo hayo itasaidia kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu haki zao za msingi na jinsi ya kuzilinda.

Laurent ameeleza kuwa hatua hiyo ni muhimu katika kuhakikisha demokrasia inaimarika na haki za binadamu zinaheshimiwa kwa kiwango cha juu.

Mafunzo haya ya uraia na utawala bora yanaendelea kuwa na mchango mkubwa katika kujenga jamii yenye uelewa wa kisera, kisheria, na kijamii, na kuwa sehemu ya jitihada za Serikali ya awamu ya sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan za kuimarisha utawala bora na maendeleo endelevu katika mikoa yote ya Tanzania.





# CCM YATAKIWA KUTOJIBU WAPINZANI

NA WILLIUM PAUL, MOSHI

WANACHAMA wa Chama cha Mapinduzi wameshauriwa kutotumia muda mwingi kuwajibu wapinzani kwani wameshapoteza dira na badala yake washuke kwa wananchi na kueleza kazi zilizofanywa na serikali chini ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Kauli hiyo imetolewa na Mjumbe wa Kamati ya Siasa ya Chama hicho mkoa wa Kilimanjaro, Adam Best Simba alipokuwa akizungumza na wanachama na wananchi wa kata ya Uru kusini wilayani Moshi ikiwa ni maadhimisho ya miaka 48 ya kuzaliwa kwa Chama cha Mapinduzi.

Alisema kuwa, serikali imefanya kazi nyingi ambazo wana ccm wanajuku ya kwenda kuzisemea kwa wananchi ili wasije kudanganywa na watu wasiolitakia mema Taifa.

"Wana CCM hatupaswi kutumia nguvu kubwa kuwajibu wapinzani kwani tayari wameshapotea kutokana na kazi kubwa ambazo zimefanyika kipindi hiki kila kata zimepelekwa fedha nyingi za maendeleo sasa jukumu letu ni kushuka kwa wananchi na kuwaeleza yale yaliyofanyika katika kipindi cha miaka minne ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan" Alisema Simba.

Mjumbe huyo wa Kamati ya Siasa alisema kuwa, mpaka sasa hakuna Chama cha kukitoa CCM madarakani na hii ni kutokana na kazi kubwa ambazo zimefanyika za kuhakikisha wanawatumikia wananchi bila kujali itikadi zao.

Katika hatua nyingine Simba aliwataka wanaccm kuhakikisha wanajiepusha na makundi ya watu ambao wamekuwa wakijipitisha na kutangaza nia za kugombea nafasi mbalimbali kwani watu hao lengo lao ni kukivuruga chama na kudai kwa sasa chama kinawatambua na kuwalinda madiwani na Wabunge waliopo madarakani.

"Kama wapo wanachama wanaotaka uongozi watambue kwa sasa muda bado wawaache viongozi waliopo madarakani wafanye kazi zao kwa mujibu wa sheria na pindi muda utakapofika ndipo watangaze nia zao" Alisema Simba.

Aidha Mjumbe huyo aliwataka wanachama kuhakikisha wanajisajili kwa kieletroniki pamoja na kulipa Ada ili kuwa wanachama hai pamoja na kuweza kufanya maamuzi katika vikao mbalimbali vya chama.

Kwa upande wake, Katibu wa CCM wilaya ya Moshi vijijini, Ramadhani Mahanyu alisema kuwa, kata ya Uru kusini ni miongoni mwa kata ambazo zimepata fedha nyingi za miradi ya maendeleo ikiwemo kituo cha Afya.

Mahanyu aliwataka wananchi kuhakikisha wanailinda miradi hiyo ili iweze kudumu muda mrefu ili lengo ambalo lilikusudiwa na serikali liweze kutimia.

Kwa upande wake, Diwani wa kata ya Uru kusini, Wilhard Kitali alisema kuwa, lipo tatizo la ubovu wa barabara ya Mama ndizi road inayounganisha vijiji vya Rau na Kariwa na kuwaomba viongozi wa chama waweze kusaidia kutatua ubovu wa barabara hiyo ambayo imekuwa kero kubwa kwa wananchi.

## CHANGAMOTO YA JESHI LA ZIMAMOTO KUPATIWA UFUMBUZI

NA MWANDISHI WETU

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Innocent Bashungwa amesema kuwa Serikali inaendelea kuliimarisha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa kulipatia vitendea kazi ambapo sasa inatekeleza mradi wa ununuzi vifaa mbalimbali vya kuzima moto na uokoaji pamoja na magari 150 ya kuzima moto na uokoaji.

Bashungwa ameeleza hayo tarehe 03 Februari 2025 wakati akijibu swali la Mbunge wa Ngorongoro, Emmanuel Shangai aliyetaka kujua Je, lini Serikali itanunua gari la Zimamoto Wilaya ya Ngorongoro.

"Kwa sasa Serikali inatekeleza mradi wa ununuzi vifaa mbalimbali vya kuzima moto na uokoaji pamoja na magari 150 ya kuzima moto na uokoaji" amesema Bashungwa

Amesema pindi magari 150 ya kuzima moto na uokoaji yatakapofika nchini, yatakayosambazwa nchi nzima ikiwemo Wilaya ya Ngorongoro.

Aidha, amesema Serikali inayoongozwa na Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan imeshaliwezesha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kununua magari 12 ya kisasa ambapo moja wapo lilitumiaka kuzima moto katika jengo gorofa la TRA Kariakoo.

Bashungwa amesema Serikali ipo mbioni kununua helikopta moja maalum kwa ajili ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ambayo yataenda sambamba na kuwapatia Mafunzo Maafisa, Wakaguzi na Askari wa Jeshi hilo.

# Mil. 468 Kuendeleza mradi wa barabara Ruvuma



NA MWANDISHI WETU

WAKALA wa Barabara za vijijini na mijini Tanzania (TARURA) wilaya ya Mbinga mkoani Ruvuma,umetenga zaidi ya Sh.milioni 468 ili kuendelea na mradi wa ujenzi wa Barabara ya Kihamili-Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya Mbinga kwa kiwango cha lami.

Ujenzi wa Barabara hiyo unalenga kuwaondolea Wananchi adha ya usafiri wanapokwenda kupata matibabu

> *"Tunaipongeza sana Serikali yetu kwa hiki inachofanya kwani ni msaada mkubwa kwetu sisi Wananchi tunaoishi hasa maeneo ya vijijini,sisi tunaridhika na kufurahi kwa kazi nzuri inayofanywa na Serikali kupitia TARURA"*

kwenye Hospitali hiyo,kurahisisha huduma ya kusafirisha mazao na kukuza kipato cha Mwananchi mmoja mmoja,wilaya ya Mbinga na Taifa kwa ujumla.

Meneja wa TARURA Wilaya ya Mbinga Oscar Mussa amesema,Barabara hiyo inajengwa kwa awamu na ina urefu wa kilometa 3.4 na kwa mwaka wa fedha 2024/2025 imejengwa kwa kiwango cha lami urefu wa mita 750.

Aidha Mussa, ametaja kazi nyingine zilizotekelezwa katika mradi huo ni pamoja na kufungua barabara mpya yenye urefu wa kilometa 3.5 kuelekea makazi mapya ya viongozi wa Halmashauri ya wilaya Mbinga.

Alisema,licha ya kurahisisha usafiri kwa wananchi watakaokwenda kupata matibabu katika Hospitali ya Halmashauri,Barabara hiyo itakuwa msaada mkubwa kwa wanafunzi na wafanyakazi wa Chuo cha Ufundi Stadi (VETA) kwenda na kurudi chuoni na kuboresha Barabara katika eneo la Kihamili ambalo ni kioo kwa kata ya Kigonsera.

"lengo kubwa la Wakala wa Barabara za vijijini na mijini(TARURA) ni kuwawezesha wananchi wa kata ya Kigonsera na wilaya ya Mbinga kwa ujumla kupata wepesi katika shughuli zao za kila siku hasa kilimo cha mzao ya chakula na biashara"alisema.

Kwa mujibu wa Mussa, kazi zilizofanyika hadi sasa ni kujenga Barabara kwa tuta kwa kiwango cha lami ambapo mkandarasi anaendelea kujenga mitaro ya kupitisha maji eneo lote la mradi na baada ya kazi hiyo ataendelea kuweka alama za barabarani na kufunga taa.

Mkazi wa kijiji cha Kigonsera Benson Chiwinga alisema,ujio wa miradi ya Barabara unawezesha vijana wengi kupata kazi zinazowapatia kipato na kupata ujuzi ambao baada ya miradi hiyo kukamilika wanautumia kuendelea kujiajiri na kuepuka kushiriki kwenye matukio ya kiharifu.

Ameipongeza Serikali kwa kuleta miradi hiyo,lakini ameomba isichoke kuendelea kuleta miradi katika Tarafa ya Kigonsera ili wananchi waweze kunufaika kwani itawasaidia kupata ujuzi na kuboresha maisha na kukuza uchumi wao.

"Tunaipongeza sana Serikali yetu kwa hiki inachofanya kwani ni msaada mkubwa kwetu sisi Wananchi tunaoishi hasa maeneo ya vijijini,sisi tunaridhika na kufurahi kwa kazi nzuri inayofanywa na Serikali kupitia TARURA"alisema Chiwinga.

Haji Mbawala alisema,awali Barabara hiyo ilikuwa mbaya kutokana na kuwa a madimbwi mengi katikati ya barabara hasa wakati wa mvua hali iliyosababisha shughuli zao za kilimo na usafiri na usafirishaji kuwa ngumu.

# TAHARIRI

## Usimvunje nguvu mkuu wa nchi anapowaza kutukomboa

KUMEKUWA na maneno ya chini chini kwenye mitandao ya jamii juu ya ziara anazofanya Rais Samia Suluhu Hassan kwenye mataifa mbalimbali duniani.

Ziara ambazo zinasaidia kuifungua nchi kimataifa, kuwapa fursa wawekezaji wa ndani kuona upeo wa dunia lakini pia kuweka mazingira mazuri ya kukaribisha wawekezaji wa nje.

Hata hivyo, wapo wanaoumizwa na ziara hizo. Kwa madai hazina maana, zinatumia fedha za walipa kodi bure bila sababu. Wanakwenda watu wengi kuliko ilivyopaswa kuwa.

Ni kauli za wakosaji, ambazo zimejaa hila, ghiba na choyo kisicho na sababu yoyote. Rais Samia Suluhu Hassan amekifanya kile ambacho viongozi wengi waliopata kukalia kiti chake nchini hawakukuweza, au walikifanya kwa udogo.

Kitendo cha kuongozana na wafanyabiashara, wanahabari, wasanii, wanamichezo, wanamazingira na watu wa kada mbalimbali katika ziara zake ni upeo wa juu wa kuwafikiria wananchi wake.

Wanapofika huko watu hao ambao baadhi wanajigharamia nauli na malazi, wanatambulishwa kwa diaspora. Wanatambulishwa kwa wafanyabiashara wakubwa au wasanii wakubwa wa nchi anazotembelea Rais Samia.

Hakuna kitu kizuri kama kupata kiongozi anayefikiria hatma ya wananchi wake, angeweza kwenda mwenyewe kimya kimya kisha akarudi kimya kimya na chochote kisitokee. Lakini ameamua kulifanya hili la kuongozana na watu bado wapo wanaomsakama.

Hatumtendei haki, kwa sababu analifanya hili si kwa kushurutishwa na hakuna namna yoyote iwayo kuwa ananufaika na kitendo hiki zaidi ya kuwa wanaokwenda naye ndio wanaonufaika.

Kama hiyo haitoshi, mbali ya ziara za kitaifa anazofanya anapata wasaa wa kufuatilia mikopo na misaada yenye masharti nafuu kwa ajili ya miradi ya maendeleo ikiwemo hospitali, miundombinu ya barabara, majengo na taasisi za elimu.


## BODI YA UHARIRI

Mhariri Mkuu:
Mhariri Habari za Biashra & Uchumi:

Mhariri wa Habari:
Idara ya Masoko:

## MAWASILIANO

JAMVI MEDIA GROUP




*Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ashiriki Maadhimisho ya Siku ya Sheria nchini ambayo Kitaifa yamefanyika katika viwanja vya Chinangali Jijini Dodoma*

# UCHAMBUZI

## Nchimbi -- mshikamano wetu ndio nguzo yetu

ANAANDIKA MSHITITI
DK. AHMAD SOVU

KAMA angekuwa mchezaji wa mpira wa miguu wa timu ya Yanga basi Dk. Nchimbi ningemuita Aziz Ki au wa Azam angekuwa Fei toto na kama ni Simba basi ndio Clatous Chama na kama ni Mashujaa basi ndio Reliants Lusajo. Maana amepiga ndipo palipo.

Kupiga huku si kupiga kwa boli hapana, ni kutoa hoja au ukumbusho katika wakati mwafaka na pahala mwafaka.

Akiwa mkoani Singida katika ziara yake ya kwanza kwa mzunguko huu wa pili wa mfululizo wa ziara zake, katibu mkuu wa CCM, Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi kwa kinywa kipana kabisa na bila kificho amekemea tabia ya baadhi ya watu wachache kutaka kutugombanisha na kuhubiri chokochoko na kauli za kibaguzi zinazoashiria kuvuruga umoja na mshikamano wetu kama taifa la Tanzania.

Alisema Dk. Nchimbi: "Tusikubali kuacha umoja wetu nawaombeni sana, kama kuna jambo mkienda nyumbani leo na mtu akikuuliza katibu mkuu amesema nini umwambie amesema tusikubali kuacha umoja wetu, tusikubali kugawanywa, tusikubali kufarakanishwa."

Kauli hii ya Dk. Nchimbi imekuja wakati mwafaka kwani ni kweli zipo bishara za baadhi ya watu kuanza maneno yanayoelekea kuuteteresha umoja wetu.

Watanzania ni wamoja na umoja na mshikamano wetu kwa hakika hauna mbadala.

Umoja na mshikamano wetu ndio umetufikisha katika hatua kubwa ya maendeleo iliyopigwa.

Tumeshuhudia mathalan, katika kipindi cha miaka mitatu tu ya Rais Dk. Samia kumepigwa hatua kubwa za maendeleo.

Uendelezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo kama vile SGR, umeme katika Bwawa la Mwalimu Nyerere, ujenzi wa miundombinu ya mwendokasi na barabara nchi nzima, ongezeko kubwa la watalii, maboresho makubwa katika sekta ya afya na elimu, maboresho katika sekta ya kilimo, uvuvi, mifugo,michezo, sanaa mawasiliano n.k ni mifano ya umuhimu wa kuwa na umoja, amani na mshikamano kama Taifa.

Hivyo, ni lazima kulinda umoja huu na mshikamano wetu na kuepuka kubaguana kwa misingi ya ukabila, dini, maeneo na matabaka kama alivyosisitiza Dk. Nchimbi kuwa;

"Tanzania lazima iendelee kuwa nchi moja yenye mshikamano, yenye upendo ambayo haibagui watu wake kwa misingi ya ukabila, wala dini wala vyama vya siasa. Wote ni Watanzania, nchi yetu sote tuishi kwa kushirikiana na tupendane."

Kwa hakika, tunatoa kongole sana kwa Balozi Dk. Nchimbi kwa kukumbusha suala hili muhimu na adhimu kwa Taifa.

Tunatoa mwito kwa viongozi wengine wa serikali, dini, vyama vya siasa na vya kijamii na wananchi mmoja mmoja kuendelea kumuunga mkono Dk. Nchimbi kwa kukumbusha na kuonya kwa yeyote atakayeashiria kutaka kuuteteresha umoja wetu.

# JINSI YA KUJIKINGA NA UGONJWA WA MARBURG




NA JIMMY CHIKA

KULINGANA na Umoja wa Mataifa, virusi vya Marburg, ambavyo ni sawa na virusi hatari vya Ebola, viligunduliwa kwa mara ya kwanza baada ya watu 31 kuambukizwa, saba kati yao walikufa, mnamo 1967 huko Marburg na Frankfurt. Ujerumani na Belgrade huko Serbia.

Virusi vya Marburg vilipatikana kwa mara ya kwanza kwa tumbili wa kijani kibichi wa Kiafrika

Mlipuko huo ulitokana na tumbili wa Kiafrika walioagizwa kutoka Uganda. Lakini virusi hivyo vimehusishwa na wanyama wengine tangu wakati huo.

Na miongoni mwa wanadamu, huenezwa zaidi na watu ambao wamekaa kwa muda mrefu katika mapango na migodi iliyo na popo.

Huu ni mlipuko wa kwanza nchini Ghana - lakini nchi kadhaa za Afrikazimewahi kuripoti mlipiko wa virusi ikiwa ni pamoja:

Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo
Kenya
Afrika Kusini
Uganda
Zimbabwe

Mlipuko wa mwaka 2005 nchini Angola ulisababisha vifo vya watu zaidi ya 300. Lakini barani Ulaya, ni mtu mmoja tu amefariki katika kipindi cha miaka 40 - na mmoja nchini Marekani,baada ya kurejea kutoka katika safari ya kuzuru mapango nchini Uganda.

Milipuko mikubwa:

2017, Uganda: visa vitatu, watu watatu walifariki
2012, Uganda: vis 15, watu wanne walifariki
2005, Angola: visa 374, watu 329 walifariki
1998-2000, DR Congo: visa 154 cases, watu 128 walifariki
1967, Ujerumani: visa 29, watu saba walifariki
Chanzo: WHO

Inasababisha ugonjwa gani?

Unaanza ghafla na:
Homa
kuumwa vibaya na kichwa
kuumwa na misuli

Hii mara nyingi siku tatu hufuatwa na:
kuharisha
kuumwa na tumbo
kichefuchefu
kutapika

WHO inasema: “Mwonekano wa wagonjwa katika awamu hii umeelezewa kuwa unaonyesha sifa za ‘kama mzimu’, macho ya ndani, nyuso zisizo na hisia na uchovu mwingi.”

Baadhi ya watu hutokwa na damu sehemu mbalimbali za mwili na kufa siku nane hadi tisa baada ya kuugua kwa sababu ya kupoteza damu nyingi na mshtuko.

Kwa wastani, virusi huua nusu ya walioambukizwa, WHO inasema, lakini aina hatari zaidi imeua hadi 88%.

Popo wa matunda wa rousette wa Misri ndiye mbebaji mkuu wa virusiChanzo cha picha,Getty Images

Maelezo ya picha,Popo wa matunda wa rousette wa Misri ndiye mbebaji mkuu wa virusi

Je, inaeneaje?

Popo wa matunda aina ya rousette wa Misri mara nyingi huwa na virusi. Nyani wa kijani kibichi na nguruwe wanaweza pia kubeba.

Miongoni mwa wanadamu, huenea kupitia maji ya mwili na malazi yaliyochafuliwa nao.

Na hata watu wakipona, damu au shahawa zao, kwa mfano, zinaweza kuwaambukiza wengine kwa miezi mingi baadaye.

Je, inaweza kutibiwaje?

Hakuna chanjo maalum au matibabu ya virusi.

Lakini aina mbalimbali za bidhaa za damu, madawa ya kulevya na matibabu ya kinga yanatengenezwa, WHO inasema.

Na madaktari wanaweza kupunguza dalili kwa kuwapa wagonjwa waliofika hospitali maji mengi ili kuchukua nafasi ya damu iliyopotea.

Vinawezaje kudhibitiwa?

Watu barani Afrika wanapaswa kuepuka kula au kushika nyama ya porini, Gavi, shirika la kimataifa linalokuza upatikanaji wa chanjo, linasema.

Watu pia wanapaswa kuepuka kuwa karibu na nguruwe katika maeneo yenye mlipuko, WHO inasema.

Wanaume ambao wamekuwa na virusi wanapaswa kutumia kondomu kwa mwaka mmoja baada ya kupata alili au hadi shahawa zao zitakapothibitishwa mara mbili kuwa hazina virusi.

Na wale wanaozika watu ambao wamekufa kutokana na virusi wanapaswa kuepuka kugusa mwili.



*Picha mbalimbali katika Maadhimisho ya Siku ya Sheria nchini ambayo Kitaifa yamefanyika katika viwanja vya Chinangali Jijini Dodoma, jana ambapo mgeni rasmi alikuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan.*









*Picha mbalimbali katika Maadhimisho ya Siku ya Sheria nchini ambayo Kitaifa yamefanyika katika viwanja vya Chinangali Jijini Dodoma, jana ambapo mgeni rasmi alikuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan.*

# MAPOROMOKO KALAMBO YAORODHESHWE URITHI UNESCO



NA MWANDISHI WETU, KALAMBO, RUKWA

MAPOROMOKO ya Maji ya Kalambo (Kalambo WaterFalls), moja ya maajabu ya asili yaliyozungukwa na uoto wa kijani kibichi na hewa safi!

Kutokana na umuhimu huu Serikali imeombwa kuorodhesha maporomoko hayo ya Maji ya Kalambo mkoani Rukwa kwenye orodha ya Urithi wa Dunia wa UNESCO ili kuchagiza utalii na kutengeneza fursa za ajira kwa vijana na wanawake mkoani humo.

Wito huo umetolewa wilayani Kalambo Januari 30,2025 na Mkurugenzi wa TAMCODE Bi. Rose Ngunangwa wakati wa ziara ya shirika hilo pamoja na waandishi wa habari iliyofanywa kwa ufadhili wa UNESCO- Alwalweed Philanthropies.

Bi. Ngunangwa amesisitiza kuwa, uorodheshaji huu utachochea ukuaji wa sekta ya utalii, kuongeza fursa za ajira, na kuboresha maisha ya wanawake na vijana mkoani Rukwa.

> Afisa Michezo na Utamaduni wa Mkoa wa Rukwa, Adam Evarist, amesisitiza umuhimu wa kuendeleza juhudi hizi za kuboresha miundombinu, huku akisema ipo haja ya kutunza mazingira ya eneo hili ili urithi huu uendelee kuwepo kwa vizazi vijavyo.

Maporomoko ya Kalambo, yenye urefu wa mita 235 (futi 772), ni ya pili kwa urefu barani Afrika, na ni moja ya sehemu chache duniani zinazozungukwa na misitu ya asili isiyoingiliwa na shughuli za kibinadamu.

Pamoja na uzuri wake wa kipekee, eneo hili linatoa nafasi kubwa ya kutangaza utalii wa kipekee na kuchangia katika uchumi wa taifa.

Mali Asilia na Fursa za Ajira

Bi. Ngunangwa ameonyesha matumaini kuwa ikiwa maporomoko ya Kalambo yatapewa hadhi ya kimataifa, yatavutia wawekezaji kutoka sekta ya umma na binafsi, na hivyo kuongeza idadi ya hoteli, migahawa, na huduma nyingine muhimu za utalii.

"Hii ni fursa kubwa kwa vijana na wanawake wa mkoa wa Rukwa kupata ajira na kuboresha hali zao za maisha. Kutangaza urithi huu duniani kote kutawawezesha kupata nafasi nyingi za kazi katika sekta ya utalii. Hivyo ni vyema Wizara ya Utalii na Maliasili ikachagiza wawekezaji kutoka katika sekta ya umma na binafsi," amesema Bi. Ngunangwa.

Miundombinu Inaboreshwa kwa Urahisi wa Kufika

Hata hivyo, changamoto ya awali ilikuwa ni miundombinu, ambapo kumekuwa na ugumu wa kufika kwenye maporomoko haya kwa asilimia mia moja. Lakini kwa sasa, serikali imejenga ngazi 1,270 zinazoshuka hadi kwenye maporomoko, na kufanya eneo hili kufikika kwa urahisi zaidi kwa watalii na wageni.

Afisa Michezo na Utamaduni wa Mkoa wa Rukwa, Adam Evarist, amesisitiza umuhimu wa kuendeleza juhudi hizi za kuboresha miundombinu, huku akisema ipo haja ya kutunza mazingira ya eneo hili ili urithi huu uendelee kuwepo kwa vizazi vijavyo.

Kutunza Misitu na Kuhifadhi Utamaduni

Ziara hii iliyofanyika mkoani Rukwa, imejumuisha waandishi wa habari kutoka vyombo vya habari vya kijamii na kidigitali, watendaji wa TAMCODE, na maafisa kutoka Manispaa ya Sumbawanga ili kuchagiza umuhimu wa kutunza misitu, utalii na urithishwaji wa utamaduni usioshikika na unaoshikika.

Wamejadili pia umuhimu wa kutunza misitu na kuendeleza urithi wa kiutamaduni unaoshikika na usioshikika.

"Tutakapolinda mazingira, tutahakikisha kwamba maporomoko haya yanatufaa kwa vizazi vijavyo, na kuwa sehemu ya urithi wa dunia," amesema Ngunangwa.

Katika mwanga wa juhudi hizi, mkoa wa Rukwa unaonekana kuwa na nafasi ya kipekee ya kuandika historia mpya ya maendeleo kupitia utalii endelevu, ambao utaongeza fursa za ajira, kuboresha uchumi wa mkoa, na kuchangia katika ustawi wa taifa kwa ujumla.

# Unaikumbuka Mk group "Ngoma za maghorofani"?



NA MWANDISHI WETU

ILIKUWA ni bendi ya Kishua kweli kweli, ili uweze kuingia kuona shoo zao, ulilazimika kuwa nadhifu Kwa mavazi na pia uwezo wa kifedha kuanzia kiingilio hadi matanuzi ya ndani.

Ni miungoni mwa bendi chache zilizokuwa zikifanya maonyesho katika hoteli kubwa na yenye hadhi kama New Africa iliyopo ubavuni mwa kituo cha Posta ya zamani.

Enzi zake maeneo hayo yalikuwa ndiyo rasmi kwa vijana wa Jiji la Dar es Salaam kufanya matembezi hasa siku za mwishoni mwa wiki.

Ukiacha burudani ya bendi hiyo iliyokuwa ikiitwa ya "Kishua" pia maeneo hayo yalikuwa karibu na majumba maarufu yanayoonyesha Sinema.

Ilikuwa jirani kabisa na ukumbi wa Empress Cinema, Empire na hata Avalon, New chox, Cameo na Odeon hayakuwa mbali, kijana angeweza kutembea Kwa miguu polepole na mpenzi wake kuelekea anapohitaji kupata burudani.

Huo ndiyo wasifu wa eneo la hoteli ya New Africa ilipokuwa ikipiga bendi ya Mk Group.

Hao ndiyo Wana Ngulupa Tupatupa dance iliyovuma zaidi wakati ilipokuwa chini ya kiongozi na mwimbaji nguli, Clayton Kasongo Mpinda.

Licha ya kupita waimbaji na wapiga magitaa wengi kama vile mwamba Mondo wa Mondondee, au mtaalamu wa masauti Paul Vitang, lakini kuna ukweli kuwa nyimbo zilizobamba zaidi za bendi hiyo ni zile zilizopigwa zama za mpiga gitaa hodari na mtunzi Joseph Mulenga alipoungana na Kasongo.



Leo tunauangalia wimbo uliokuwa ukiwatoa machozi mashabiki wa Mk group uitwao Maumivu Makali, utunzi wake Mulenga akiuwakilisha mazoezini kipindi ambacho bendi hiyo ilikusanya wachapakazi wenye vipaji katika kila eneo.

Radha ya nyimbo za Mk group zilinoga kutokana na mchanganyiko wa wanamuziki waliotoka katika bendi mbalimbali ambako nako wakifanya kazi iliyokamata vilivyo.

Usisahau kuwa enzi hizo bendi zilihitaji wapiga vinanda mahiri Kwa bahati nzuri Mk group wakafanya umafia na kumnasa Lister Elia.

Lister ndiyo aliyeleta mapigo ya kinanda cha kisasa enzi hizo akibadilisha kutoka vile vilivyozoeleka vya akina Waziri Ali ( Msondo), Kassim Magati (Bima), Farahani Mzee (Mwenge) nk.

Kama ilivyo ada Mulenga naye akawa ni zaidi ya mwanamuziki kwani magitaa yake huko Mlimani park yalikuwa yakiendelea kuwatesa wanamuziki aliowaachia kijiti.

Hebu tuangalie wimbo wa Maumivu Makali ambao licha ya kubamba vilivyo lakini pia ulikuwa katika albam iliyopendwa zaidi na mashabiki.

Katika albam hiyo kulikuwa na nyimbo na watunzi kama ifuatavyo

(Mapenzi ya adhabu) utunzi wake Luster Elia), Mariam Marie (Kasongo Mpinda), Adaria (Mbombo wa Mbomboka) Mbelaombwe (Shem Karenga), Maumivu makali (Mulenga) na Rosa alioutunga (Issa Nundu).

Muda mfupi baada ya albam hii kurekodiwa Mk group ilishuhudia idadi ya mashabiki kuongezeka katika maonyesho yao ndani ya hoteli ya kitalii New Afrika, ghorofa ya 7.

Wakati bendi hiyo ikikamata vilivyo, ilikuwa na kikosi kazi hatari kama kifuatacho.

Safu ya uimbaji iliongozwa na Kasongo Mpinda, Mbombo wa Mbomboka, Paul Vitangi na Issa Nundu.

Trampet zilipulizwa na Abdalah Tuba, Kayembe Ndalambu na Tromblow Musimbi.

Kinanda Lister Elia, Solo Joseph Mulenga, Ridhim Omar Makuka, Besi Joseph Mapega, Dram Mathei Joseph na Tumba Siddy Morris.

# CCM Tabora wasafiri na Dkt. Samia, Dkt Mwinyi

NA ALLAN KITWE, JAMHURIMEDIA, TABORA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Mkoani hapa kimeunga mkono uamuzi wa Mkutano Mkuu wa CCM Taifa kuwapitisha Dkt Samia Suluhu Hassan, Dkt Hussein Mwinyi na Dkt Nchimbi kuwa wagombea Urais kupitia CCM mwaka huu.




Pongezi hizo zimetolewa na Viongozi mbalimbali wa chama hicho kwenye maandamano ya amani yaliyofanyika juzi mjini hapa ambapo walieleza kuwa hatua hiyo imetokana na kasi na weledi mkubwa walioonesha katika utendaji wao.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Tabora Said Mkumba amesema kuwa wamefanya maandamano hayo ili kuunga mkono uamuzi huo kwa kuwa viongozi hao 2 wameonesha uwezo mkubwa na kusimamia kwa asilimia 100utekelezaji ilani.

ëUamuzi huo ni ishara tosha kwamba wanaCCM tumeridhishwa na uwezo wao na kasi yao ya kusimamia utekelezaji ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020-2025 kwa asilimia 100 na tuna imani kubwa kwaoí, ameeleza.

Amebainisha kuwa uamuzi huo unamaanisha kwamba Rais Samia na Mgombea mwenza Dkt Nchimbi ndio chaguo la wanaCCM kwenye urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais Mwinyi kwenye urais wa Zanzibar.

Nkumba ameeleza kuwa kasi ya maendeleo yaliyoletwa na Rais Samia na Rais Mwinyi kule Zanzibar ni kielelezo tosha kuwa Viongozi hawa wanatosha kupewa mitano tena na huo ndio uamuzi wa mwisho wa wanaCCM wote.

ëRais Samia ni mwanamke shujaa na kiongozi makini mwenye maono makubwa ya kimaendeleo, tumepokea uteuzi huo kwa mikono miwili, Tabora tunaunga mkono mapendekezo hayo kwa asilimia 100í, amesema.

Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Mohamed Nassoro amesema kuwa CCM ni chama imara na kitaendelea kuchagua Viongozi makini, wazalendo, wachapa kazi, wanaojali watu na siyo maslahi binafsi na wenye kauli safi.

Amebainisha kuwa Rais Samia, Rais Mwinyi na Emanuel Nchimbi ni chaguo sahihi, wana kila sifa zinazotakiwa na watanzania wote na wameonesha uwezo mkubwa katika utendaji wao.

ëWatanzania wana kila sababu ya kuwashukuru wajumbe wa Mkutano Mkuu kwa maamuzi hayo ambayo yatawapa nafasi



Inaendelea Uk. 13

# CCM Tabora wasafiri na Dkt. Samia, Dkt Mwinyi

Inatoka Uk. 12



wagombea hao wa CCM kujipanga vizuri kwa ajili ya uchaguzi mkuu utakaohusisha vyama vya upinzanií, amesema.

Naye Katibu wa CCM Mkoa Wilson Nkambaku ameeleza kuwa wajumbe wa Mkutano Mkuu wameonesha ukomavu mkubwa wa kisiasa na huo ndio ukweli, hata katiba ya chama inawapa nafasi ya kuendelea kushika nafasi hiyo.

Amebainisha kuwa wapinzani hawajawa na uwezo wa kuongoza nchi, hivyo akawataka kuendelea kujifunza kwa Chama Cha Mapinduzi hadi watakapokuwa na uwezo wa kujisimamia huku akiongeza kuwa serikali ya CCM itaendelea kuwaletea maendeleo wananchi pasipo kujali itikadi zao.

&&&

Mbunge wa Jimbo la Shinyanga Mjini, Patrobas Katambi, amesoma taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) 2020/2024, akisema ameitekeleza kwa asilimia 100.

Taarifa hiyo aliwasilisha leo Januari 24, 2025, mbele ya Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM Jimbo la Shinyanga Mjini, ambapo Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Wazazi CCM Taifa, Ally Hapi, alikuwa mgeni rasmi.

Katambi, ambaye pia ni Naibu Waziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu), amebainisha mafanikio katika sekta mbalimbali, ikiwemo elimu, afya, miundombinu, maji, na nishati safi ya kupikia.

Elimu

Mbunge Katambi amesema ndani ya miaka minne, shule mpya tisa zimejengwa, zikiwemo shule za msingi tano na sekondari nne. Aidha, alifanikiwa kuanzisha tawi la Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo na kupanua Chuo Kikuu cha Moshi (KICoB) tawi la Kizumbi.

Miundombinu

Katambi ameeleza kuwa miundombinu ya barabara, madaraja, na masoko imeboreshwa. Alitaja ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Ibadakuli, daraja la Uzogole, na maboresho ya barabara katika maeneo ya Iwelyangula, Ibinzamata, Ndala, Ihapa, Mwamalili, na Mwanoni.

Afya

Ameboresha huduma za afya kwa kujenga vituo vya afya, zahanati sita, na hospitali, ikiwemo Kituo cha Afya Kambarage na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Shinyanga. Pia, alitoa ambulensi sita kwa msaada wa Rais Samia Suluhu Hassan.

Maji

Amesema mtandao wa maji umeongezwa katika maeneo ya Bugwandege, Masekelo, Mwamasheke, Mwanubi, Busongo, na maeneo ya mjini. Zaidi ya shilingi bilioni 195 zimetengwa kwa usambazaji wa maji kwa kipindi cha 2024/2025.

Mikopo na Ajira

Ameeleza kuwa shilingi milioni 200 zilitolewa kwa vikundi vya Boda boda, Bajaji, wanawake, na watu wenye ulemavu kupitia Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga. Pia, milioni 19 zilipatikana kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu.

Nishati Safi

Katambi amegawa mitungi ya gesi 1,780 kwa makundi mbalimbali ili kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia.



Michezo

Mbunge huyo alianzisha ligi mbalimbali za michezo, ikiwemo utoaji wa zawadi za hadi shilingi milioni 6 kwa washindi wa mashindano.

Katambi amewataka wana-CCM kushirikiana kwa ajili ya maendeleo na kuepuka migogoro. Aliwasihi viongozi wa chama kuendelea kushirikiana kwa manufaa ya wananchi.

Katibu wa CCM Mkoa wa Shinyanga, Odilia Batimayo, amempongeza Katambi kwa kazi nzuri na alionya dhidi ya kampeni za mapema za kugombea ubunge. Ally Hapi naye alimsifu Katambi kwa utekelezaji mzuri wa Ilani ya CCM, akisema mafanikio hayo yanaongeza imani ya wananchi kwa chama.

Hapi amewataka wagombea kuzingatia maadili ya chama, kujiepusha na wapambe wa kisiasa, na kuendeleza siasa za kisayansi kwa kujenga hoja kwa wananchi.

Katika hafla hiyo, Katambi pia amekabidhi kiti mwendo kwa mtoto mwenye ulemavu, Delfina Mashaka, na vifaa vya sauti kwa uongozi wa Stendi ya Mabasi ya Mkoa wa Shinyanga.

# MASHABIKI SIMBA WATAMBA NA TIMU YAO

>> Inatoka uk. 16

pande hizi mbili, ambapo Yanga walitamani kuona mtani wao akipoteza mechi hiyo ili wafanane na matokeo waliyokumbana nao hao katika mechi ya Ligi Kuu mzunguko wa kwanza ambapo Tabora United iliwachapwa mabao 3-1.

Hata hivyo simba ilionyesha kuukamia mchezo huo ikipeleka idadi kubwa ya mnashabiki kutoka Jijini Dar es Salaam, akiwemo Mdhamini Mkuu wa zamani wa klabu hiyo Azim Dewji ili kuhakikisha wanaondoka na Pointi zote tatu.

Baada ya kumalizika kwa mchezo huo mashabiki wa Simba wakijivunia ushindi huo, walianza kuwatambia wenzao wa Yanga waliokuwemo uwanjani humo, wakidai kuwa timu yao ndiyo iliyoonyesha staili yao ya 'Gusa Achia' tofauti na hao wenyewe walioibuni.

Kwa ushindi huo, Simba SC ilifikisha pointi 43 na kurejea kileleni ikiwazidi pointi moja mabingwa watetezi, Yanga baada ya wote kucheza mechi 16.

Tabora United kwa upande wao walibaki na pointi zao 25 katika mechi 16, huku wakisalia kwenye nafasi ya tano.



# YANGA - POINT TATU ZA SIMBA TUNAZITAKA

>> Inatoka uk. 16

kwao, Uwanja Ali hassan Mwinyi.

Mabao ya Simba mawili yalifungwa na Lionel Ateba pamoja na Shomari kapombe aliyepigilia msumari wa mwisho. Lakini pamoja na matokeo ya Simba yaliyowafanya warejee kileleni wakiwazidi watani wao wa jadi kwa Pointii 1, Simba ikifikisha 43 na Yanga 42, Wanajangwano hao wamedai kuwa matokeo hayo wala hayawatishi kwa vile safari yao ya kuelekea kutetea ubingwa wao ipo palepale.

Meneja Habari wa Yanga Ali Kamwe alithibitisha kuwa hata kama timu hizo zitaendelea kuchuana kwa idadi ya Pointi, lakini anaamini watakapokutana nao itaongeza pointi tatu kutoka Msimbazi.

# RASHFORD UYOO ASTONVILA

BARCELONA, HISPANIA

WAWAKILISHI wa mshambuliaji wa Manchester United, Marcus Rashford wamekutana na viongozi wa Antonvila siku ya Jumanne huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 akitafuta njia ya kuondoka ndani ya kikosi hicho.

Rashford kumekuwa na uvumi wa kutakiwa na timu kadhaa, hivyo kuzidi kufanya uvumi wa kuondoka kwake kushika kasi zaidi, huku hayo yakija wakati Paul Scholes akisema, ndani ya kikosi hicho kuna wachezaji wanane wabovu.



# LUIZ ANAKWENDA HAPA

MILAN, IITALIA

TIMU ya Juventus wameipa Chelsea fursa ya kumsajili kiungo wa kati wa Brazil Douglas Luiz, 26, ambaye pia ananyatiwa na Manchester City na Arsenal.

Hayo yaja huku kiungo wa Ufaransa Paul Pogba, 31, anazingatia ofa kadhaa kutoka kwa timu za ligi tano kuu za Ulaya, lakini makubaliano ya mkataba hayajafikiwa.




# P-SQUARE 'Mapacha' ndani ya mgogoro!-3

LOGOS, NIGERIA

NI lazima ieleweke kwamba mashabiki hawakupenda P-Square kwa sababu ya nani aliimba au kucheza zaidi. Kilichotufanya tufanikiwe ni ubora wetu hali yetu iliotokana na juhudi zetu za pamoja – sisi wawili! P-Square ilikuwa ya nguvu, na mashabiki waliipenda P-Square kwa sababu ya upekee wetu na umoja, "aliongeza.

Pia alimkosoa Paul kwa kujilinganisha na Jude, akisema kuwa mienendo ya familia ilikuwa na jukumu kubwa katika matatizo ya bendi. "Ulimvunjia heshima mke wangu, familia yangu, kipaji changu, mawazo yangu na hata kuchukua upande wa Jude wakati alipokuwa anajaribu kunikandamiza."

Katika kukamilisha ujumbe wake, Peter alielezea kusikitishwa kwake na hali ya sasa na athari ambayo P- Square imekuwa nayo kwa mashabiki wao. "Sasa nahisi kama umechukua mambo hata zaidi kwa kujaribu kuwageuza mashabiki dhidi yangu kwa kuwafanya wafikiri nina wivu kwako. Umefanya kila kitu unachoweza kuwafanya mashabiki wanichukie, lakini unajua nini? Hawatanichukia kamwe; badala yake, watatuchukia sisi sote kwa sababu tuliwavunja moyo na kuwaangusha."

# DRAKE AFICHUA SIRI YA MAFANIKO YAKE



LOS ANGELES, MAREKANI

SUPASTAA wa muziki wa Hip hop, Drake, amesema siri ya mafanikio yake ni kujifunza kutoka kwa waliofanikiwa.

Drake mwenye umri wa miaka 38, amesema tangu alipokuwa mdogo, alipenda kufuatilia maisha ya mastaa na kuvutiwa na hatua zao kwenye maisha.

Mshikaji huyo mzaliwa wa Toronto, alianza rasmi safari yake ya muziki mwaka 2006 kupitia 'mixtape' yake ya 'Room for Improvement.'

# Tamasha la muziki 'Kadanse ya Mama' yakumbusha enzi za Gurumo na Bitchuka

NA MWANDISHI WETU

TAMASHA la Muziki wa dansi lililoitwa Kadanse ya Mama lilifanyika juzi Jumamosi katika Viwanja vya Ledrs Kinondoni Jijini Dar es Salaam na kushudiwa na umati wa mashabiki huku bendi zaidi ya kumi zikitumbuiza.

Miungoni mwao ni bendi kongwe Msondo Ngoma Music Band iliyoazishwa tangu mwaka 1964 pamona na Mlimani Park iliyozaliwa mwaka 1978, bendi hizi zilipitiwa na wanamuzki mbalimbali wakiwemo maarufu Muhidin Maalim Gurumo ambaye ameshatangulia mbele ya haki na Hassan Rehani Bitchuka ambaye kwa sasa amepumzika masuala ya muziki.

Wanamuziki hao wanakumbukwa kutokana na kila bendi kati ya hizo mbili kuwa na wanamuziki wanaonakiri sauti zao na hivyo kusikika kama wakongwe hao walikupo jukwaani.

Ttukiacha historia ndefu ya jinsi waimbaji wawili nguli Muhidin Gurumo na Hassan Bitchuka walivyokutana kwa mara ya kwanza mwaka 1973 katika bendi ya NUTA Jazz, baadaye wakakutana tena katika miaka na bendi tofauti, lakini mkutano wao wa mwaka 1991 ulikuwa na kishindo kikubwa.

Mwaka huu miamba hii ilikutana tena katika bendi ya Juwata Jazz, hii ni baada ya misele ya kuingia na kutoka mfano kwenda Mlimani park na kisha Orchestra Safari Sound, hapa walikutana tena.

Tena basi katika mkutano huo mabingwwa hawa wa uimbaji hawakuwa hao wawili tu, bali waliwakuta wenzao waliokwisha jijingea mahaba makubwa kwa mashabiki kutokana na uwezo wao wa kuimba na pia tungo zao bora.

Katika safu ya uimbaji pia alikuwepo TX Moshi William, Joseph Maina, Juma Akida, Isaya Swahiba, Athuman Momba, Joseph Lusungu na Hamisi Kitambi.

Kipindi hicho Juwata jazz 'Wanamsondo ngoma' ilikuwa ikihudumiwa na wanamuziki takriban 28 wakiwemo na mafundi mitambo.

Tarehe 5.9.1991 bendi hii ilikuwa imekamilisha mazoezi ya nyimbo 9, na kuingia Studio za RTD kwa ajili ya kuzirekodi.



Tanzania BORA
MICHEZO
tanzaniabora @tanzaniabora @tanzaniabora
JUMANNE Februari 04, 2025
Tovuti: www.tanzaniabora.co.tz



UK. 15

# Mashabiki Simba watamba na timu yao



NA MWANDISHI WETU

MASHABIKI wa Simba wanadai kuwa kikosi chao ndicho kinachocheza 'Staili' ya 'Gusa Achia' inayotumiwa na watani wao wa jadi Yanga, hivyo wamewataka wajifunze kupitia timu yao, endapo wanatamani kuona wanachokisema ndicho wanachotenda.

\Hizo ni tambo za watani hao wa jadi, zilizosambaa kwa kasi mjini Tabora, wakati kikosi cha Simba kilipoivaa Tabora United na kuibuka na ushindi mnono wa mabao 3-0.

Mchezo huo ulikuwa ukifuatiliwa kwa karibu na mashabiki wa

Inaendelea Uk.14

## YANGA - POINT TATU ZA SIMBA TUNAZITAKA

NA MWANDISHI WETU

KLABU mahasimu wa soka la Bongo Simba na Yanga, wamemaliza wikiendi yao vizuri kwa kila moja kupata ushindi mnono uliozidi kuwaimarisha katika msimamo wa Ligi Kuu ya NBC.

Ilianza Yanga iliyovuna ushindi wa mabao 4-0 ikiichapa bila huruma Kagera Sugar, mchezo uliopigwa Jumamosi kwenye Uwanja wa KMC Mwenge Jijini Dar es salaam.

Mabao ya Yanga yalifungwa na mshambuliaji Clement Mzize dakika ya 32, kiungo Mudathir Yahya dakika ya 60, kiungo, Pacome Zouzoua kwa Penalti kunako dakika ya 78 na mshambuliaji Mzambia, Kennedy Musonda aliyefunga dakika ya 86, kwa kichwa.

Jumapili ikawa zamu ya Wekundu wa Msimbazi ambao nao walikamilisha Kalamu yao wakiishindilia Tabora United jumla ya mabao 3-0, wakifanya mauaji hayo nyumbani

Inaendelea Uk.14



## PSG, ARSENAL ZATAJWA VITA YA GOMA

NA MWANDISHI WETU

JAMUHURI ya Kidemokrasi ya Congo imeziandikia timu za soka barani Ulaya zinazopata ufadhili kutoka serikali ya Rwanda kutopokea, 'Fedha zinazotokana na umwagikaji wa damu,' unaoendelea mashariki mwa DRC.

Hayo yamekuja baada ya vita kali inayoendelea katika mji wa Goma ukihusisha kundi la waasi wa M23, wanaoendesha mauaji




na uporaji katika eneo hilo na kuhatarisha usalama wa raia.

Kulingana na DRC, Waziri wake wa mambo ya kigeni Therese Kayikwamba Wagner ameziandikia klabu za Arsenal FC ya Uingereza, Paris Sint-Germaine ya Ufaransa na FC Bayern Munich ya Ujerumani kusitisha ushirikiano wao wa ufadhili wa mauzo

Inaendelea Uk.15

GAZETI HILI HUTOLEWA NA JAMVI MEDIA GROUP, S. L. P 78862, DAR ES SALAAM